

## Rahabu ni nani?

Jina “**Rahabu**” limeonekana mara kadhaa katika biblia likiwa na maana Zaidi ya moja. Maana ya kwanza ni linamwakilisha Mwanamke wa kikanaani aliyekuwa kahaba, aliyewahifadhi wapelelezi wa kiisraeli walioingia kuipeleleza Yeriko, na maana ya pili Taifa la Misri.

Kama tu vile neno “**Mharabu**” katika biblia linamaanisha Jamii ya watu wa Arabia, lakini pia linamaanisha “*Mtu au Malaika anayeharibu* Vivyo hivyo na jina Rahabu lina maana Zaidi ya moja.

### **1.RAHABU (Kahaba).**

Habari ya Rahabu aliywakuwa kahaba tunaipata katika kitabu cha *Yoshua mlango wa 2 na wa 6*. Mwanamke huyu aliwahifadhi wapelelezi wa kiisraeli walioingia Yeriko kuipeleleza nchi ile.

*Yoshua 2:1 "Yoshua, mwana wa Nuni, akawatuma watu wawili kutoka Shitimu kwa siri, ili kupeleleza, akawaambia, Enendeni mkaitazame nchi hii, na Yeriko. Wakaenda wakafika nyumbani kwa kahaba mmoja jina lake aliiitwa Rahabu, wakalala huko.*

*2 Mfalme wa Yeriko akaambiwa, kusema, Tazama, watu wawili wa wana wa Israeli wameingia humu leo usiku, ili kuipeleleza nchi.*

*3 Mfalme wa Yeriko akatuma watu kwa Rahabu, akasema, Watoe watu wale waliokuja kwako, walioingia ndani ya nyumba yako, maana wamekuja ili kuipeleleza nchi.*

*4 Yule mwanamke akawatcaa wale watu wawili, akawaficha, akasema, Naam, wale watu walikuja kwangu, lakini sikujua walikotoka"*

## **2.TAIFA LA MISRI.**

Jina Rahabu pia katika biblia limetumika kuwakilisha Joka kubwa la baharini ambalo ufunuo wake ni Taifa la Misri.

*Isaya 30:7 "Kwa maana Misri huwasaidia bure, bila faida; Kwa hiyo nimemwita, Rahabu aketiye kimya"*

*Isaya 51:10 "Si wewe uliyemkata-kata Rahabu? Uliyemchoma yule joka? Si wewe uliyekausha bahari, Na maji ya vilindi vikuu; Uliyevifanya vilindi kuwa njia, Ili wapite watu waliokombolewa?"*

*Zaburi 87: 4 "Nitataja Rahabu na Babeli Miongoni mwao wanaonijua. Tazama Filisti, na Tiro, na Kushi; Huyu alizaliwa humo"*

Soma pia Ayubu 26:12, na Zaburi 89:10..

Jambo kubwa na kuu tunaloweza kujifunza kwa **RAHABU** (*Aliyekuwa Kahaba*) ni **IMANI**.

Alikuwa na Imani juu ya mambo yatarajiwayo sawasawa na *Waebrani* 11:1. Aliziamini nguvu za MUNGU wa Israeli, hivyo akajua yatakayofuata baadaye kuwa ni anguko la Yeriko, hivyo akatafuta njia ya

kujinusuru yeye na familia yake kwa kujiungamanisha na jamii ya Israeli.

*Waembrania 11:31 “Kwa imani Rahabu, yule kahaba, hakuangamia pamoja na hao walioasi; kwa kuwa aliwakaribisha wale wapelelezi kwa amani”.*

*Yakobo 2:25 “Vivyo hivyo na Rahabu, yule kahaba naye, je! Hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, hapo alipowakaribisha wajumbe, akawatoa nje kwa njia nyininge?*

*26 Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa”.*

Maran atha.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link

hii >> <https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx>

## 10

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:  
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au  
Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

**Mafundisho mengine:**

**RAHABU.**

**LAANA YA YERIKO.**

**Kwa maana kahaba ni shimo refu; Na malaya ni rima jembamba.**

**Je! Daudi hakuwa mtoto wa ndoa wa Yesu? (Zab 51:5)**

**FAHAMU MAISHA YA YESU KABLA YA HUDUMA.**

**Rudi nyumbani**

Rahabu kwenye biblia.

Share on:

WhatsApp

[Print this post](#)